

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI  
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



UZALISHAJI WA MBEGU BORA AU VIPANDO  
VYA MALISHO.



Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)  
Kampasi ya Morogoro  
S.L.P. 603,  
MOROGORO – TANZANIA  
E-mail: [litamorocamp@gmail.com](mailto:litamorocamp@gmail.com)

### Utangulizi

Mbegu ni sehemu ya mmea ambayo hutumika kwa ajili ya kuotesha au kustawisha malisho ambayo ni nguzo kuu ya uzalishaji wa mifugo. Uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora au vipando vya malisho ni jambo la msingi ili kufanikisha kilimo cha malisho.

### Makundi ya mbegu za Malisho

- Mbegu,



- Vishina,



- Pingili pingili



- Miche.



### UMUHIMU WA MBEGU

Mbegu ni pembejeo muhimu sana katika kilimo cha malisho. Umakini unatakiwa katika kuzalisha mbegu bora ili kuboresha kilimo hiki. Hivyo basi sekta ya mbegu huweka kanuni za uzalishaji mbegu ili kuhakikisha vigezo vya ubora wa mbegu vinazingatiwa na wadau wote.

### FAIDA ZA KUTUMIA MBEGU BORA

- Ongezeko la mavuno ya malisho
- Uwezo wa mbegu kuota unaongezeka
- Kutokuwa na maambukizo ya magonjwa.
- Matumizi ya pembejeo kama mbolea, madawa n.k yanatumika kwa faida kuongeza mavuno
- Mbegu bora husaidia kuzalisha mimea, itakayozalisha mbegu bora msimu unaofuata.